

TAARIFA YA MRADI UJENZI WA MZANI MWALONI KIRUMBA KWA KAMATI YA SIASA MKOA WA MWANZA

UTANGULIZI

Mwalo wa Kirumba una upekee wake kwa kuwa, tofauti na mialo mingine, eneo hili ni soko mama la kibiashara ambalo hupokea mazao ya samaki na jamii yake ya ziwa Victoria kutoka sehemu mbalimbali, ndani na nje ya Manispaa ya Ilemela na nchi kwa ajili ya kuuzwa.

Manispaa iliona ni vyema kuupa kipaumbele kwa kufunga mzani kutokana na changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika ukusanyaji wa mapato ukizingatia kuwa, sheria ndogo ya tozo za ushuru wa samaki na mazao yake ya mwaka 2014 ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inatutaka tutoze kwa kilo na wala sio kwa kukisia kwa kuangalia ukubwa wa gunia kama ilivyokuwa ikifanyika.

Katika bajeti ya mwaka 2017/18, Halmashauri ilitenga jumla ya Tshs. 260,712,819 kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa mzani katika soko la samaki la kirumba. Kazi hii inafanywa na kampuni ya M/S Great Lakers ya Mwanza. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 22/11/2017 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 22/02/2018. Hata hivyo, mradi huu haukukamilika kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwemo kubadili eneo la ujenzi ambako kulisababisha kuongezeka ukubwa wa kazi kutokana na aina ya udogo. Hadi sasa, utekelezaji uko asilimia tisini (90%) na unatarajiwa kukamilika mwezi huu.

FAIDA TARAJIWA ZA MRADI

Mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuleta faida zifuatazo;

- Halmashauri na serikali kuu kukusanya fedha nyingi iliyokuwa ikipotea kutokana na kukadiria uzani wa mzigo.
- Kwa kufunga mzani licha ya kutoa huduma kwa wafanyabiashara wetu, pia tumelenga kufanya biashara ya kupima uzito wa mizigo wa magari mengine makubwa hasa ukizingatia pale kwa kishimba kila gari hutoza zaidi ya Tsh. 15,000/=
- Matakwa ya sheria za nchi katika kutoza ushuru wa mazao yanatutaka tutoze katika ujazo wa kilo na wala si kwa kudhania tu, hivyo itatusaidia kuondoa migogoro na wafanyabiashara, na taasisi nyingine za serikali zinazosimamia tozo na uzani wa mizigo.
- Zaidi ya yote ni kuboresha takwimu zetu ambazo kimsingi husaidia sana katika kufanya maamuzi mbalimbali ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla juu ya Sekta yetu ya Uvuvi.